HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA KILIMANJARO-MAWENZI

S.L.P 3054

MOSHI

04 Januri,2022

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA KUJITOLEA

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kilimanjaro –Mawenzi inatangaza nafasi **40** za ajira ya kujitolea katika kada mbalimbali, watakao ajiriwa kwenye nafasi hizi watalipwa nusu ya mshahara wa Serikali (TGOS,TGHOS,TGHS na TGS) wa cheo husika.

1. **Afisa Tehama Msaidizi Daraja la II-Nafasi -1**
   awe wenye Stashahada katika moja ya fani ya Uhandisi wa Kompyuta/ Mitandao/ Mawasiliano na Elektroniki au Matengenezo ya mifurno ya TEHAMA kutoka kwenye Taasisi/Vyuo vinavyotarnbuliwa na Serikali..

2. **Afisa Tehama Daraja la II-Nafasi -1**
   awe wenye Shahada katika moja ya fani ya Uhandisi wa kompyuta/ mitandao/ mawasiliano na Elektroniki au Matengenezo ya mifurno ya TEHAMA kutoka kwenye Taasisi/Vyuo vinavyotarnbuliwa na Serikali..

3. **Mteknolojia Mionzi Daraja II – (Radiografa) Nafasi-1** awe wenye Stashahada katika fani ya Mteknolojia Mionzi kwa muda wa miaka mitatu katika fani ya radiolojia kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kimesajiliwa

4. **Daktari Daraja la II- Nafasi – 4,** awe wenye Shahada ya Udaktari kutoka chuo Kinachotambuliwa na Serikali waliomaliza mafunzo ya kazi"Internship" ya muda usiopungua miezi kum i na miwili na kupata usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika).

5. **Afisa Ustawi wa Jamii Daraja la II- Nafasi 1,** awe wenye Shahada ya Ustawi wa Jamii kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

6. **Afisa Lishe Daraja la II - Nafasi 1,** awe wenye Shahada ya kwanza ya lishe, Sayansi Kimu na Lishe, au Sayansi ya Chakula na teknolojia ya Chakula, Home Economics and Nutrition, Food Science and Technology kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali

7. **Daktari wa Meno Daraja la II - Nafasi 1** awe wenye Shahada ya Udaktari wa Meno kutoka Vyuo Vikuu/Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali waliomaliza mafunzo ya kazi"Internship" ya muda usiopungua miezi kumi na miwili na kupata usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika).

8. **Afisa Afya Mazingira Msaidizi II - Nafasi 1,** awe mwenye Stashahada ya Sayansi ya Afya ya Mazingira ya miaka mitatu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali na awe amesajiliwa na Bodi ya Wataalamu wa Afya Mazingira.

*Scanned by TapScanner*

9. ***Mteknolojia Madawa Daraja II – Nafasi 3*** *awe* wenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia Madawa ya muda wa miaka mitatu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza ya Wafamasia.

10. **Mteknolojia Madawa Msaidizi – Nafasi 1**, *awe* wahitimu wa kidato cha nne wenye cheti cha miaka miwili katika fani Madawa kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali

11. **Mhudumu wa Afya Chumba cha Maiti– Nafasi 2** awe wahitimu wa kidato cha nne waliopata mafunzo ya mwaka mmoja katika fani ya chumba cha maiti.

12. ***DOBI – Nafasi 2*** *awe* wenye wahitimu wa kidato cha nne waliofuzu mafunzo ya miaka miwili au mitatu katika fani ya Dobi (Laundry Services) kutoka katika vyuo vinavyotambulika na Serikali.

13. **Msaidizi wa Hesabu Daraja la I (Accounts Assistant I)-Nafasi 6** awe wenye Stashahada ya Uhasibu kutoka chuo kinachotambulika na Serikali AU mwenye Cheti cha ATEC II kinachotolewa na NBAA.

14. **Afisa Hesabu Daraja la II (Accounts Officer II) – Nafasi 1** awe wenye "Intermediate Certificate" (Module D) inayotolewa na NBAA au sifa nyingine zinazolingana na hizo, Shahada ya Biashara/Sanaa aliyejiimarisha kwenye fani ya Uhasibu. kutoka Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali.

15. **Afisa Ugavi Daraja la II (Supplies Officer II) - Nafasi 1** awe wenye Shahada/ Stashahada ya juu ya Ununuzi/Ugavi kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali
    AU wenye "Professional level III" inayotolewa Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi nchini (Procurement and Supplies Professionals and Technicians Board - (PSPTB) au sifa nyingine inayolingana na hiyo inayotambuliwa na PSPTB, na kusajiliwa na PSPTB kama "Graduate Procurement and Supplies Professional".

16. **Afisa Ugavi Msaidizi (Assistant Supplies Officer II) - Nafasi 1** awe na Stashahada (Doploma) ya Ununuzi/Ugavi au Biashara iliyojiimarisha katika Ununuzi na Ugavi, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, au sifa inayolingana na hizo inayotambuliwa na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi nchini (Procurement and Supplies Professionals and Technicians Board - (PSPTB).

17. **Wasaidizi wa Kumbukumbuku Daraja la II - Nafasi 4** awe na Astashahada/Stashahada ya Utunzaji wa kumbukumbu katika masuala ya afya (medical records) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

*Scanned by TapScanner*

18. **Afisa Mwaadazi/Mpishi Daraja la III – Nafasi 2** awe mhitimu wa kidato cha nne waliofuzu mafunzo ya miaka miwili katika fani ya Catering & Hotel Managementi kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

19. **Fundi Sanifu Msaidizi (fundi Mbomba) Daraja la II- Nafasi 1** awe wenye elimu ya kidato cha nne na mafunzo ya mwaka mmoja kutoka chuo cha maji au chuo kinachotambuliwa na Serikali na wanatoa cheti cha ufundi daraja la III.

20. **Fundi Sanifu (Umeme) Daraja la II- Nafasi 1** awe wenye elimu ya kidato cha nne aliyehudhuria na kufaulu mafumzo ya mwaka mmoja ya fundi umeme kutoka chuo cha Veta au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

21. **Dereva Daraja la II - Nafasi 3,** awe wenye elimu ya kidato cha nne (IV) leseni ya class E1,D1,C1 Awe na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda wa mwaka 1 bila kusababisha ajali, Awe amehudhuria mafunzo ya msingi wa kuendesha magari ( Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (veta) au chuo kinachotambulika na serikali

22. **Afisa Habari Daraja la II - Nafasi 1** awe wenye shahada katika fani ya sanaa ya sayansi au aliyefunzu mafunzo ya awali ya uandishi wa habari (Mass Comunication)

Waombaji wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

(i) Awe Mtanzania
(ii) Awe na cheti cha ufaulu cha kidato cha nne au cha sita
(iii) Awe na Cheti cha ufaulu cha taaluma husika
(iv) Awe na Cheti cha kuzaliwa
(v) Curriculum vitae (CV)
(vi) Awe na umri usiozidi miaka 45

Barua za maombi zitumwe Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kilimanjaro-Mawenzi kwa anuani ifuatayo:-

Mganga Mfawidhi
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kilimanjaro-Mawenzi
S.L.P 3054
**MOSHI**

Mwisho wa kupokea maombi ni **Tarehe 20 Januari, 2022 saa 9:30** Alasiri

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA MAWENZI
S.L.P. 3054 MOSHI

Dkt. Edna- Joy Munisi
**MGANGA MFAWIDHI**
**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA KILIMANJARO-MAWENZI**

*Scanned by TapScanner*